**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

# TAARIFA KWA UMMA

## KUHUSU UCHAGUZI MDOGO WA UDIWANI KATIKA KATA YA MASOKO JIMBO LA MBEYA VIJIJINI NA KATA YA NDONO JIMBO LA UYUI

**Dodoma, 21 Novemba, 2025**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea taarifa kutoka kwa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuhusu kifo cha; -

1. **Ndugu Sephania Katesi Better,** Diwani mteule wa Kata ya Masoko Jimbo la Mbeya Vijijini kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilichotokea tarehe 02 Novemba, 2025; na
2. **Ndugu Thabiti Mrisho Ally,** Diwani mteule wa Kata ya Ndono Jimbo la Uyui kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilichotokea tarehe 10 Novemba, 2025.

Taarifa hizo zimetolewa kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 106(2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024.

Aidha, kutokana na vifo hivyo na kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 61(1) na (3), 68(2) na 106(2) vya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024, Tume inatoa taarifa kwa umma kuhusu ratiba ya uchaguzi mdogo wa Udiwani katika Kata ya Masoko Jimbo la Mbeya Vijijini na Kata ya Ndono Jimbo la Uyui kama ifuatavyo: -

1. Fomu za uteuzi kwa wagombea Udiwani, Kata za Masoko na Ndono zitatolewa **tarehe 25 Novemba, 2025 hadi 01 Disemba, 2025;**
2. Uteuzi wa wagombea Udiwani, Kata ya Masoko na Ndono utafanyika **tarehe 01 Disemba, 2025;**

3. Kampeni za uchaguzi wa Udiwani, Kata ya Masoko na Ndono zitafanyika kuanzia **tarehe 02 Disemba, 2025 hadi 29 Disemba, 2025;**

4. Uchaguzi mdogo wa Udiwani, Kata ya Masoko na Ndono utafanyika **siku ya Jumanne tarehe 30 Disemba, 2025.**

Tume inatumia nafasi hii kuvikumbusha vyama vya siasa, wagombea na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi, Taratibu, Miongozo na Maelekezo ya Tume katika kufanikisha ratiba ya uchaguzi husika.

Imetolewa na:

Kailima, R. K
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**